Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ulioitishwa na kufanyika tarehe 19 mwezi 9 mwaka 2007 mbele ya:

..............................................
BIBI KUDRA J. MWINYIMVUA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi*

L.S.

..............................................
MHE. SALIM M. KIBONGE,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi*

NAKUBALI,

..............................................
Dodoma, MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB.),
18 Mei, 2009 *Waziri Mkuu*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 248 la tarehe 24/7/2009

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 na 13*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI, 2009

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, 2009, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.



2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, maneno yafuatayo yatakuwa na maana iliyoelekezwa hapa;

"Ada/ushuru" maana yake ni malipo yanayotozwa na kulipwa kwa ajili ya huduma zinazotolewa na Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi au mtumishi mwingine wa Halmashauri ambaye atateuliwa kukaimu nafasi hiyo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

4.–(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya bidhaa au huduma zinazotolewa kwa malipo katika eneo lake, huduma hizo zikijumuisha utoaji wa vibali na leseni mbalimbali kama inavyoonyeshwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kabla ya kupata huduma inayohusika au vinginevyo kama itakavyoelezwa na Halmashauri kwa maandishi.

5. Mtu ye yote anayewajibika kulipa ada ama ushuru atalipa kabla ya kupata huduma kama inavyoonyeshwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi.

6.–(1) Ada na ushuru unaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi italipwa kwa Halmashauri au wakala wake ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha malipo hayo.

(2) Ni wajibu wa mtu ye yote anayelipa ada au ushuru kudai na kuhakikisha anapewa stakabadhi kwa malipo anayotoa.

7. Isipokuwa malipo ya ada zinazolipwa kwa muda maalum, ada zote na ushuru utalipwa kabla ya kutoa au kupokea huduma.

8.–(1) Mtu yeyote anayepaswa kulipa ada au ushuru akishindwa kufanya malipo hayo katika muda unaostahili Halmashauri inaweza kukusanya ada au ushuru huo wa njia ya Mahakama.

(2) Bila ya kuathiri masharti yanayotajwa na kifungu kidogo cha (1) hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada au ushuru kwa njia ya kukamata na kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na ada au ushuru anaodaiwa, kiasi hicho kikihesabiwa pamoja na gharama za zoezi la ukamataji na usafirishaji wa mali hiyo.

(3) Halmashauri itauza kwa mnada mali yo yote iliyokamatwa chini ya kifungu hiki iwapo;

(a) baada ya siku thelathini (30) tangu mali kukamatwa mdaiwa atakuwa hajalipa ada ama ushuru anaodaiwa, pamoja na gharama za ziada anazopaswa kulipa;

(b) mali iliyokamatwa inaweza kuharibika haraka, ndani ya kipindi kisichizidi siku mbili za kalenda;

(c) mmiliki wa mali iliyokamatwa hatakuwa amejitokeza ndani ya siku kumi na nne baada ya mali yake kukamatwa.

9. Halmashauri haitawajibika kwa hasara yo yote na kwa namna yo yote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali zitakazokamatwa na kushikiliwa chini ya fungu la 8 la Sheria Ndogo hizi.

10.Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, matumishi ye yote wa Halmashauri au wakala anaweza kuingia katika jengo lo lote kwa nia ya kukusanya ada au ushuru katika muda wa kawaida wa kazi, au wakati mwingine wo wote kama itakavyoamriwa na Mkurugenzi.

11.–(1) Litakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu ye yote;

(a) kukataa au kushindwa kutii agizo lo lote atakalopewa na Mkurugenzi kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru;

(b) kumzuia Afisa wa Halmashauri au mtu ye yote mwingine aliyeruhusiwa kukusanya ada au ushuru katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi;





(c) kukwepa kwa makusudi kulipa kiwango cha ushuru anachostahili kulipa;

(d) kushawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ushuru.

(2) Mtu ye yote atakayepatikana na hatia chini ya Sheria Ndogo hizi atalipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) na isiyozidi laki moja (100,000/=), au kifungo kisichopungua miezi sita jela, au vyote viwili, kifungo na faini.

## NYONGEZA YA KWANZA

### SEHEMU A

ADA ZA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA

(i) Gari dogo la abiria....................................Shilingi 1,500 kwa siku
(ii) Gari kubwa la abiria..................................Shilingi 2,000 kwa siku
(iii) Gari dogo la mizigo..................................Shilingi 2,000 kwa siku
(iv) Gari kubwa la mizigo................................Shilingi 2,500 kwa siku

### SEHEMU B

ADA ZA KULAZA MAGARI KATIKA YADI YA HALMASHAURI (KWA USIKU MMOJA)

(i) Magari madogo ya watu binafsi.............................shilingi 2,500
(ii) Magari makubwa ya binafsi (Lori au basi).............shilingi 4,000
(iii) Machine na mitambo ya ujenzi wa barabara...........shilingi 5,000
(iv) Pikipiki...............................................................shilingi 1,000

### SEHEMU C

ADA YA VIBAO VYA MATANGAZO KWA MWAKA

(i) Mabango yasiyong'ara (kwa kila sqm)..................................................3000/=
(ii) Mabango yanayong' ara (kwa kila sqm)...............................................5000/=
(iii) Mabango ya biashara (yanayodumu kwa hadi siku saba))................10,000/=
(iv) Mabango ya biashara (yanayodumu kwa hadi siku 14)......................25,000/=
(v) Mabango ya biashara (yanayodumu kwa zaidi ya siku 30)...............35,000/=
(vi) Matangazo ya biashara kwa kutumia sauti (kwa siku moja).............15,000/=

## SEHEMU D

ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA KATIKA MACHINJIO YA HALMASHAURI

(i) Ng'ombe.......................................................2,500/=
(ii) Mbuzi..........................................................1,500/=
(iii) Kondoo.......................................................1,500/=
(iv) Nguruwe......................................................2,000/=

## SEHEMU E

ADA YA KUKODI UKUMBI WA HALMASHAURI (KWA SIKU MOJA)

(i) Matumizi ya ukumbi kwa semina za mashirika na miradi............40,000/=
(ii) Matumizi ya shughuli zinazofanywa na asasi za kiraia.................50,000/=
(iii) Matumizi binafsi........................................................50,000/=
(iv) Kukodi viti (kila kiti)....................................................150/=

## SEHEMU F

(i) Ada ya magobore (kwa mwaka)....................................5000/=

## SEHEMU G

ADA NA USHURU MWINGINE

(i) Ada ya kuandikisha magari ya abiria kwa mwaka
  (a) teksi.....................................................................10,000/=
  (b) mabasi madogo (hiace).................................................20,000/=
  (c) Mabasi makubwa (ya kati na makubwa)...........35,000/=
(ii) Ada ya uzio wa majengo yanayoendelea kujengwa (kwa mita moja)....100/=
(iii) Ada ya uzoaji taka (kwa kilo moja ya taka ngumu)...........................100/=
(iv) Ada ya uzoaji wa taka (kwa kilo moja ya taka laini).........................150/=
(v) Ushuru wa bima.......................................................2.5% ya makusanyo





## NYONGEZA YA PILI

## HATI YA KUKAMATA MALI NA KUIUZA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI

*(Imetengenezwa chini ya Sheria Ndogo ya 21)*

JINA LA MALI: ..........................................................................................

KWA DALALI WA MAHAKAMA

..........................................................

..........................................................

..........................................................

..........................................................

Hii ni kukuamuru kukamata na kuitunza mali inayoondosheka ya .................................................................................ambayo imeonyeshwa katika Jedwali, mpaka hapo mtajwa hapo juu atakapolipa shilingi ........................................ ikiwa ni deni la ushuru analodaiwa na riba kwa kiwango cha asilimia moja (1%) kwa kila mwezi kuanzia tarehe ........................................ mwezi ...............................mwaka ............................................. mpaka tarehe ..................................................mwezi ..........................mwaka ............................................. Ikiwa ni pamoja na gharama za kukamata mali hiyo. Na baada ya kutoa taarifa (notice) ya siku kumi na nne ambayo itabandikwa katika jengo la mahakama na baada ya kumalizika kwa notisi hiyo, mauzo ya mali hiyo yataanza kwa mnada ili kupata shilingi ............................................ Pamoja na riba na gharama za kukamatia mali hiyo.

UNAAMRIWA kurudisha hati hii mnamo au kabla ya tarehe ...............................mwezi ................................... Mwaka ...............................Pamoja na maelezo ya namna ulivyotekeleza mali hiyo.

Imetolewa na mimi na kugongwa mhuri wa Mahakama leo tarehe .......................mwezi ..............................Mwaka ......................................

..........................................................................

HAKIMU

*Tangazo la Serikali Na. 248 (linaendelea)*

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi umebandikwa kati Sheria Ndogo hii katika Kikao chake kilichoitishwa na kufanyika tare 19 mwezi 9 mwaka 2007 na umebandikwa katika Sheria Ndogo hii mb ya:

..................................

BIBI KUDRA J. MWINYIMV
*Mkurugenzi Mten*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kili*

L.S.

..................................

MHE. SALIM M. KIBON
*Mwenye*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kili*

NAKUBALI,

..................................

Dodoma,
18 Mei, 2009

MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (M
*Waziri Mk*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 249 la tarehe 24/7/2009

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu namba 7 na 13*

SHERIA NDOGO (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA Y
KILINDI, 2009

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo (Ushuru wa Madini) z Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, 2009.

2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na zitatumika katika eneo lote la Halmashauri.